**JAMHURI YA MUUNGANO**

**WA**

**TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO

# KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Julai, 2026**
**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule 0782586468/0717402768**
**Makamu Mkuu wa Shule 0712362417/0682825963**

**Shule ya Sekondari Ilulu**

**S.L.P.139 kilwa masoko**

**....................................**

**Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi……….……………………………………………..**
**S.L.P……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**:** **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ILULU ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA MKOA WA LINDI MWAKA …………**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Ilulu mwaka……….tahasusi ya………., kumbuka kuwa hii ni bahati kubwa na ya pekee kwake.

Shule ya Sekondari Ilulu iko wilayani Kilwa mkoani Lindi. Shule ipo umbali wa mita **mia tatu (300)** kutoka kituo cha basi cha kijiji cha Njia nne. Unaweza kufika shuleni kwa kutokea Dar es salaam au Lindi/Mtwara kwa kutumia usafiri wa basi. Kutokea Dar es salaam usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi Mbezi/Mbagala Rangi Tatu na utawaambia wakushushe kijiji cha Njia nne. Tumia usafiri bodaboda hadi kufika shuleni kwa Tshs **1,000/= tu**

Muhula wa masomo utaanza kulingana na taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……………………..** pamoja na barua hii, pokea,

(a) Fomu ya kupimwa afya ya mwanafunzi. Apimwe kwenye Hospitali ya Serikali, hakikisha anapimwa na sio kujaziwa fomu tu, na umwelekeze Mganga matatizo ya afya aliyonayo

(b) Fomu ya kuonesha ndugu/jamaa wa karibu, ikiwa na anuani, namba ya simu na mahali anakoishi.

(c) Fomu ya ahadi ya kutekeleza wajibu.

Kwa kumalizia, nakutakia maandalizi mema na safari njema kuja kujiunga nasi.

(MOTTO“ELIMU KWA MAENDELEO”)

**N.B**

**HAKIKISHA UNAKAMILISHA TAARIFA ZOTE MUHIMU ZINAZOHITAJIKA KUANZIA KARATASI YA 12-15. USIJE NA FOMU AMBAYO HAIJAJAZWA.**

1. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Mwanafunzi aje na sketi mbili za rangi ya kijivu iliyoiva **kitambaa kizito**. Sketi zake ziwe ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la chini la sketi zisizidi sentimita 18 au inchi $7^1/_2$. Zingatia vipimo.

ii. Sketi zake ziwe na (belt) mkanda , upana wa belt usizidi sentimeta 5 au inchi moja na nusu.

iii. Mshono wa sketi ni linda box ( Linda kubwa mbele na nyuma). Tazama mfano wa picha hapo chini

iv. Gauni la kazi za nje la kitambaa kizito (SHAMBA DRESS) rangi ya blue ya kawaida mshono wa solo ya kuunga. Kama anavaa hijabu nayo ashone rangi ya blue sawa na gauni. Gauni ziwe ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la chini ya gauni isizidi sentimita 18 au inchi $7^1/_2$. Zingatia vipimo.

**Tazama mfano wa picha hapo chini yenye rangi**





A; SHAMBA DRESS

(GAUNI YA KUSHINDIA)

B; UNIFORM

(SARE YA SHULE)

v. Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatieni vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi/shamba dress kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa, atarudishwa nyumbani ili aje na sare zilizoelekezwa

vi. Mwanafunzi anaweza kushona idadi ya sare kadri ya uwezo wake. Ila inashauriwa awe na angalau sare za darasani mbili na gauni za kazi mbili.

**N.B**

**KWA MZAZI/MLEZI ATAKAYEHITAJI SARE ZA SHULE ZINAPATIKANA KWA GHARAMA ZIFUATAZO:-**

i. **Sketi kwa moja kwa gharama ya Tshs 30,000/= n a gauni moja kwa gharama**

**Tshs 40,000/ = kwa wasiovaa hijabu**

**ii. Gauni moja kwa gharama ya Tshs 48,000/= kwa wanaovaa hijabu (gauni na hijabu).**

Aidha mwanafunzi anapaswa kuwa na sare zifuatazo:-

(i) Shati (blauzi) nyeupe mbili (2) au zaidi mikono mifupi tetroni—Tomato

(ii) Soksi nyeupe jozi mbili (2)au zaidi

(iii) Kwa wanafunzi wa kiislamu Nusu kanzu pamoja na hijabu ya tetroni nyeupe ya kitambaa cha halua na sio mtandio, isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi.

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu (kamba) (VISIWE NA VISIGINO VIREFU) jozi mbili.

(v) Track suite isiyobana na isiyokua na maandishi rangi ya blue bahari. Iwe na michirizi rangi nyeupe. Inapatikana shuleni kwa shilingi elfu ishirini na tano (25,000/=) kwa atakayehitaji

(vi) T- shirt rangi nyeusi aina ya manga (round color ) isiyo na maandishi kwa ajili ya shughuli za michezo.

(vii) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo

(viii) Aje na T-shirt rangi ya njano yenye kola ya ufito mweusi na njano pia

anaweza pata t-shirt kwa atakayehitaji kwa gharama ya Tsh 14.000/=

(ix) Aje na Sweta rangi ya damu ya mzee lenye muundo wa V mbele na anaweza kulipata shuleni kwa mzazi atakayehitaji kwa gharama ya Tshs16,000/=

**NB:** Fedha ya T-shirt , sweta, Tracksuit na sare za shule ( kama utashona shuleni ) iletwe mkononi (cash) isiingizwe bank.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Aje na sanduku (sanduku la bati) linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake.

ii. Godoro futi $2^{1/2}$x6 , kwa kuepuka mizigo unaweza kuja kununua godoro jipya **ndani ya shule** kwa sh.50,000/= tu kwa atakayehitaji

iii. Shuka za kulalia jozi (pair) mbili za futi $2^{1/2}$x6 ,rangi ya bluu bahari isiwe na maua. Shuka nzito zinapatikana shuleni kwa shilingi elfu tisa (9,000/=)tu kwa kila moja kwa atakayehitaji

iv. Aje na vifaa vya usafi binafsi kama mswaki,sabuni n.k

v. Aje na Mto na Foronya yake ya bluu bahari (kwa anayetumia).

vi. Aje na neti nyeupe ya kitanda cha futi $2^{1/2}$x6.

vii. Aje na Taulo moja (1).

viii. Aje na Nguo za ndani za kutosha;

ix. Aje na Kandambili kwa ajili ya kuogea.

x. Aje na Viatu vya plastiki rangi yoyote vya kushindia(crocks)

xi. Ndoo ndogo mbili(matumizi yake binafsi bwenini). Ndoo zinapatikana shuleni kwa shilingi elfu tano tu kwa kila moja (5,000/=) kwa atakayehitaji

xii. Aje na bakuli la mfuniko lenye vyumba (partition), kikombe na kijiko (vyombo vya chakula)

xiii. Aje na chupa ya maji ya kunywa awapo darasani

xiv. Aje na Daftari ( kaunta books) quire three saba

xv. Mathematical set moja(1)kwa matumizi yake awapo darasani kwa michepuo ya HGL, CBG na HGK.

xvi. Kwa wanafunzi watakaosoma BAM ni vizuri wanunue non programmable Scientific Calculator (**MS 991) na** Graph pad moja (1) kwa wanaosoma geography na masomo ya sayansi

xvii. Aje na Dissecting kit (kwa wanaosoma Biology)

xviii. Koti la maabara jeupe kama linalovaliwa na madaktari kwa mchepuo wa CBG

xix. Vitabu vya ibada kwa mujibu wa dhehebu lake.

xx. Aje na nakala halisi (original) ya results slip ya kidato cha nne

xxi. Aje na nakala (kopi) ya cheti cha kuzaliwa

xxii. Kama una bima ya afya njoo nayo. Kama huna bima ya afya njoo na pesa kiasi cha shilingi elfu hamsini na mbili (52,000/=) tu, kwa ajili ya bima kubwa ya NHIF.

**Nguo nyingine**

- Aje na khanga au kitenge doti moja tu.
- Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule,
- Mwanafunzi atavaaTrack Suit wakati wa maandalio ya jioni il ikujizuia na mbu.
- Mwanafunzi anaweza kuja na nguo za kulalia (night dress)

## 2.3 MICHANGO MBALIMBALI

**A ) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

*Michango yote itumwe kwenye akaunti ya shule namba 70103200012 Benki ya NMB (Ilulu Secondary School —Development account) na mwanafunzi afike na risiti halisi (Original) ya Benki..*

**B) Ream mbili (02) za karatasi kwa mwaka (zote PLAIN)**

**C) VIFAA VYA USAFI KWA WANAFUNZI WOTE**

Wanafunzi wa tahasusi zote waje na vifaa vifuatavyo

i. Soft broom moja (fagio laini la ndani)
ii. Hard broom moja (fagio gumu la chooni)
iii. Drier moja ( squizer )
iv. Dawa ya chooni lita 5.Au uje na Tsh 10,000/= utapata lita 5 shuleni

**Pia aje na vifuatavyo vya ziada kulingana na tahasusi yake kwa ajili ya usafi**

- HGL-*Panga na Brashi ngumu* yenye mpini mfupi wa mbao, kwa ajili ya kusafishia sinki la choo. Asilete yenye mpini wa plastic.
- CBG &HKL- Alete jembe lenye mpini
- HGK-Alete fyekeo na ufagio wa chelewa wa wima wa kufagilia nje

MUHIMU: Kwa mzazi atakayehitaji vifaa vyote vya usafi kwa mwanafunzi mmoja gharama yake ni 32,000 tu vinapatikana shuleni.

**NB:** VIFAA VYOTE VYA USAFI, VIFAA VYA DARASANI, DAWA YA CHOONI,GODORO ,SHUKA,NDOO, TRAKI SUTI,TSHIRT NA SWETA VINAPATIKANA DUKA LA SHULE UNAWEZA UKALETA AU UKAJA KUNUNUA HUKU.

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

**ii. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.**

iii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iv. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

v. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

vi. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vii. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;

viii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

x. Kutunza mali za shule;

xi. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kunyoa nywele kwa mtindo wowote ule(panki, kisahani, kiduku n.k). Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera yaTaifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA 2026.

Mimi (mwanafunzi)……………………………………nakutaarifu kuwa nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondar iIlulu. NIMEKUBALI/NIMEKATAA nafasi hii baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.

Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mleziwangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilulu. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa

kwa ujumla.

Jina la mwanafunzi …………………………………….

Saini…………………………………………………………

Tarehe ……………………………………………………

FOMU NAMBA 1.

To the Medical Officer

……………………………………………………………………………….

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION
TO……..……………………………………………

Please examine the above named pupil and give us the report regarding her suitability for undertaking secondary school studies.

1. Blood…………………………………………………………………………….
2. Stool…………………………………………………………………………
3. T.B.Test…………………………………………………………………………
4. Syphilis Test…………………………………………………………………………….
5. Urine Examination…………………………………………………………………
6. Eye Test…………………………………………………………………………….
7. ChestTest ………………………………………………………………………..
8. EarsTest………………………………………………………………………
9. Spleen………………………………………………………………………….
10. Abdomen………………………………………………………………………
11. Pregnancy…………………………………………………………………

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g.Physical defects or impairment, infection,family diseases etc.

……………………………………………………………………………………

I certify that, the above student is suitable/unsuitable for secondary school studies.

If unsuitable please give reasons:

……………………………………………………………………………………

Name of Medical Officer ....................................................Signature……………..

Date:………………………………          Official stamp………………………………

FOMU NAMBA 2.

1.TAARIFA ZA ANAKOTOKA MWANAFUNZI

Mkoa………………..……………………Wilaya……………………………

Tarafa……………………………………….Kata…………………………

Mtaa/Kijiji……………………………………………

Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa……………………………..………….Saini………………….

Tarehe……………………………….Mhuri…………………………….Simu……

2. MICHEZO ANAYOPENDELEA

| Na | Jina la mchezo |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

3. NAFASI YOYOTE YA UONGOZI ALIYOWAHI KUSHIKA

| Na. | Aina ya uongozi | Shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo

NB: Pamoja na fomu hizi ambatanisha na kopi ya cheti cha kuzaliwa na nakala halisi ya matokeo.

Jina la Mwanafunzi ........................................................... Saini………………

Tarehe ……………

FOMU NAMBA 3.

TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi
……………………………………………………………………………………….

Kazi………………………………………………………………………………

Anuani........................................ Namba ya simu………………………..

Mkoa…………………………Wilaya………………………..Tarafa…………..…

Kata………………………………………Mtaa/Kijiji………………………………

2. NDUGU/JAMAA WA KARIBU WA MWANAFUNZI

| Na. | JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |

Mimi Mzazi/Mlezi wa..................................................................nina ahidi Kushirikiana na walimu pamoja nawatumishi wote wa Shule ya Sekondari Ilu katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria,kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

Jina la Mzazi/Mlezi...................................Saini ................Tarehe……………….

**N.B: TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUMHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USIFANYE CHOCHOTE , NI VYEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA TAARIFA SAHIHI. NAMBA ZIPO JUU YA FOMU**